

**Maelekezo ya Kufika Chuoni**

Chuo kipo KM 5 kutoka Morogoro Mjini au KM 8 kutoka stendi ya mabasi Msamvu uelekeo wa njia ya zamani ya DSM (old DSM road) kuelekea Bigwa na kipo kandokando ya milima Uluguru.

**Hali ya Hewa**

Chuo kipo mazingira mazuri kandokando ya mlima. Hali ya hewa ya hapa chuoni ni ile ya "Coastal mountainous" na hali ya joto ni kuanzia nyuzi joto 19°C hadi 30°C. Kipindi cha mvua ni kuanzia mwezi Februari hadi Mei.

**Masomo yanayofundishwa**

Chuo hiki cha Morogoro kinachukua wanachuo wa Stashahada ya Ualimu wa Sekondari kwa masomo ya Sayansi na Lugha.

**Motto wa Chuo**

WATU WAPASWA KUFAHAMU

# KARIBU SANA CHUO CHA UALIMU MOROGORO






**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

## CHUO CHA UALIMU MOROGORO

**S.L.P 691, MOROGORO**

SIMU: +255 260 3867 Au
+255786 647323 Au
+255713620350

E-Mail: morogorotc@gmail.com
morogorotc@moe.go.tz
Blog: www.motcoict.blogspot.com
Website: www.morogorotc.ac.tz


## FOMU YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI MWAKA 2023/2024

**Ndugu, ……………………………………………..**

**MAAGIZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI YA SAYANSI,HISABATI NA TEHAMA 2023/2024**

**1.0 UTANGULIZI**

Ninayo furaha kukujulisha kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekuchagua kujiunga na Chuo hiki kwa mafunzo ya Stashahada ya Ualimu wa Sekondari. Kozi hii ni miaka miwili.

**1.2 MAAGIZO YA JUMLA**.

Ili uweze kusajiliwa unatakiwa kuzingatia yafuatayo:

a) Uwe na vyeti halisi (Original Certificates) vilivyotolewa na BARAZA LA MITIHANI tu, pamoja na nakala zake (photocopies) kwa kidato cha nne (CSEE) na vyeti vya kuhitimu (leaving certificates).

b) Uwe na barua ya kujiungana chuo iliyosainiwa na Mkuu wa Chuo.

c) (Cheti cha Afya kilichosainiwa na Daktari wa Hospitali ya Serikali-Fomu imeambatishwa.

d) Rimu moja ya karatasi A4 **(photocopy papers)**

**1.3 MAAGIZO YANAYOHUSU FEDHA**

**(i) Ada**

a) Ada ya Mafunzo ni Sh. **450,000/=** kwa mwaka. Unaweza kulipa nusu **225,000/=** kwa muhula.

**(ii) Michango**

b) Mchango wa Usajili na kitambulisho Tshs. 20,000/= Mwaka wa kwanza tu

c) Mchango wa huduma ya kwanza Tsh10,000/= kwa mwaka

d) Serikali ya wanachuo Tshs. 5,000/= kwa mwaka

e) Ulinzi Tshs. 30,000/= kwa mwaka

f) Ukarabati TShs. 25,000/= kwa mwaka.

g) Michezo Tshs. 30,000/= Kwa mwaka.

h) Vifaa vya Usafi TShs. 20,000 kwa mwaka

i) Kukodi godoro TShs. 10,000/= kwa mwaka.

j) BIMA ya Afya Tsh. 50,400/= kwa Mwaka (Lazima)

**Jumla ya michango yote ni TShs. 200,400/= kwa Mwaka**

**ADA YA CHUO INALIPWA KWA KUTUMIA CONTROL NUMBER. WASILIANA NA MHASIBU WA CHUO KWA NAMBA 0784 843653 AU 0713 620350 KUPATA CONTROL NUMBER YA KULIPA ADA.**

**MICHANGO YOTE ILIPWE CRDB**: Jina la Akaunti - **Morogoro Teachers' College. Akaunti No. 01J1076984900.**

Uje na Pay In Slips (Original). Usisahau kuandika jina lako kwenye Pay In slips unapoweka fedha benki.

**NB: MWANACHUO ASIYEKAMILISHA MALIPO YA ADA NA MICHANGO HATAPOKELEWA CHUONI.**

**1.4 SARE YA CHUO.**

**Kila mwanachuo anatakiwa kuwa na sare kama ifuatavyo.**

**(i ) WANAWAKE:**

- Mashati mawili mikono mirefu-Light Blue
- Suti nyeusi mbili za heshima (angalia mchoro wa Sketi ulioambatishwa)
- Viatu vyeusi vyenye visigino vifupi
- Tai mbili nyeusi fupi
- Koti jeupe la Maabara (Wanaosoma Physics, Chemistry na Biology)
- Kwa Waislam-Hijab rangi ya light blue
- Socks nyeusi

**(ii) WANAUME:**

- Mashati mawili mikono mirefu – Light Blue
- Suti nyeusi mbili (Angalia mchoro wa Suruali ulioambatishwa). Koti vifungo viwili
- Viatu vyeusi vya ngozi
- Tai mbili nyeusi ndefu.
- Koti jeupe la maabara (Wanaosoma Physics, Chemistry na Biology)
- Soksi nyeusi

**1.5 MAHITAJI MENGINE**

a) Uje na blanketi, shuka mbili za pinki au light blue, mto na foronya, pia chandarua.

b) Daftari (counter book) kumi (10), matematical seti, calculator na vitabu vya Taasisi ya Elimu Tanzania kulingana na masomo yake.

c) Vyombo vya chakula kama sahani /kikombe

d) ***Uje na kadi ya Bima ya afya kama unayo. Kama huna hakikisha umelipa Bima ya afya kwani chuo hakitagharamia matibabu ya mwanachuo nje ya Huduma ya kwanza itolewayo chuoni.***

**1.6 VIFAA VYA MICHEZO**

a) Tracksuit ya Bluu yenye ufito mweupe pembeni (Chuoni zinapatikana kwa Tshs. 20,000/=)

b) T-Shirt itanunuliwa Chuoni. Uje na Tsh. 15,000/=

c) Raba nyeusi za michezo na soksi zake

d) Jezi ya rangi ya blue au nyeupe moja.

**1.7 KUWASILI CHUONI**.

Unatakiwa kufika chuoni tarehe **17/07/2023.** Mwisho wa kuripoti Chuoni ni tarehe **31/07/2023.**

Unashauriwa kukodi tax ili ufike salama chuoni. Hii ni kwa sababu chuo kipo umbali wa Km. 8 kutoka kituo cha mabasi MSAMVU. Gharama ya kukodi Tax wastani ni sh.10,000/= hadi 15,000/= toka MSAMVU hadi CHUONI. Kwa usalama wako ukifika usiku tafadhali chukua Taxi ndani ya kituo cha mabasi siyo nje ya kituo.

1.8 **MAMBO MUHIMU UKIFIKA CHUONI**.

Ufikapo chuoni pitia hatua zote za kusajiliwa kama ifuatavyo:

a) Jiandikishe ufikapo lango kuu

b) Onana na Msajili na uoneshe vyeti kama ulivyoagizwa. Rejea No.1.2 na Pay Inn Slips ulizolipia ada na michango.

c) Msajili akithibitisha kuwa umekamilisha maagizo yote muhimu atakusajili na kukukabidhi kwa Mwadili ambaye atakupangia Bweni.

d) Huruhusiwi kwenda Bwenini bila kusajiliwa.

1.9 Maelekezo muhimu kuhusu mafunzo yako na taratibu za Chuo yatatolewa wakati wa maelekezo ya awali (orientation) ukifika chuoni.

1.10.Ukifika utakabidhi sheria za chuo, ambazo utatakiwa kuzisoma na kuzielewa, na kisha kuzisaini mbele ya Mzazi/Mlezi kabla ya kuwasili chuoni.

1.11 Vyeti vyako vitahakikiwa na jopo MAALUM. Kwa hiyo jiridhishe mwenyewe kuwa vyeti hivyo ni halisi na halali

**KARIBU SANA CHUONI MOROGORO**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU MOROGORO
S. L. P 691, MOROGORO

**AUGUSTINE J. SAHILI**
**MKUU WA CHUO**

**Nakala:**

Mkurugenzi Msaidizi - Ualimu,
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 10,
**40479 DODOMA.**

**GOVERNMENT OF TANZANIA**

**PART A**: **REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

TO: The Medical Officer,

………………………………………………
………………………………………………
………………………………………………

From: **The Principal,**
Morogoro Teachers' College,
P. O. Box 691,
**MOROGORO.**

**12/06/2023**

**Mr/Miss/Mrs**………………………………………………………………………………… (Name in Full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full-time teacher training course. The examination should include the following categories (I – IV) each category or sub-category of which will render the applicant ineligible in case of defect.

Pregnancy (Category IV) will also render a girl ineligible for the course.

i) (a) Eye-sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Venereal Diseases
(e) Leprosy
(f) Limbs
(g) Epilepsy

ii) Neuroses
iii) Other serious diseases
iv) Pregnancy

---

**PART B:** **MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a Government Medical Officer)
I have examined the above named and considered that he/she is physically and mentally fit/unfit for a full-time teacher training course.


a) Eye-sight ……………………………………………………………………………………………
b) Hearing ……………………………………………………………………………………………..
c) Limbs ……………………………………………………………………………………………….
d) Venereal diseases……………………………………………………………………………………
e) Leprosy ……………………………………………………………………………………………..
f) Epilepsy……………………………………………………………………………………………..
g) Neuroses ……………………………………………………………………………………………
h) Other serious diseases ……………………………………………………………………………..
i) Pregnancy ………………………………………………………………………………………….

Date ………………………………… Signature ………………………………………..


Station ……………………………… Designation ………………………………………

Official stamp

**MUONEKANO (MSHONO) WA SARE ZA CHUO KWA WANAWAKE NA WANAUME**



**SKETI** ndefu ya Heshima ivuke magoti zaidi ya inchi 5.



**SURUALI** – isiwe fupi au ya kubana. Upana wa Chini (hem) inchi 16.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

**CHUO CHA UALIMU MOROGORO**

**S.L.P 691, MOROGORO**

e-mail: **morogorotc@gmail.com; morogorotc@moe.go.tz**

**MABORESHO YAMEFANYIKA LEO** **TAREHE: 12/06/2023**

## SHERIA ZA CHUO

Sheria hizi ni mwongozo wa namna ya kuishi na kuenenda kwa Wanachuo wote wa Chuo cha Ualimu Morogoro wawapo Chuoni na nje ya Chuo. Hivyo, ni lazima kwa mujibu wa sheria za Chuo kila Mwanachauo kupata nakala ya sheria za Chuo. Aidha, Mwanachuo anapaswa kuweka sahihi na kurudisha nakala ya sheria iliyosainiwa kwa Mwadili wa Wanachuo.

1. **Ruhusa kwa Wanachuo**

**a.** Ruhusa kwa Mwanachuo yeyote kwenda nje ya Chuo muda wa masomo zitatolewa na Mkufunzi wa zamu. Aidha ruhusa zote za kulala nje ya Chuo zitatolewa na Mkuu wa Chuo kupitia Ofisi ya Uadili. Hivyo, ni marufuku kwa Mwanachuo kuondoka Chuoni au kusafiri kwa muda mfupi au mrefu pasipo ruhusa.

*Mwanachuo atakayefanya kosa la kwenda nje ya Chuo bila ruhusa kutoka Ofisi husika, kuchelewa kurudi Chuoni atapewa adhabu itakayopangwa ikiwa ni pamoja na onyo au kusimamishwa masomo kwa muda usiozidi siku kumi na nne (14). Aidha kwa Mwanachuo yeyote atakayeondoka Chuoni kwa muda wa wiki moja na kuendelea bila ruhusa atasimamishwa masomo kwa muda usiozidi siku ishirini na moja (21).*

b. Mwanachuo yeyote atakayekutwa katika mazingira ya Chuo bila kibali cha maandishi juu ya uwepo wake kutoka uongozi wa Chuo wakati angali akitumikia adhabu ya kusimamishwa Chuo kwa muda ikiwa haijakoma atakuwa katenda kosa

*Mwanachuo wa aina hii atapewa onyo kwa maandishi na adhabu ya kusimamishwa itaanza upya.*

2. **Utoro kwa Wanachuo**.

Ni kosa kwa mwanachuo kutohudhuria vipindi vya masomo darasani bila sababu yoyote ile ya msingi au kibali maalumu kutoka kwa viongozi (ofisi ya taaluma/mkufunzi wa zamu).

*Mwanachuo atakayebainika kwa kosa hilo la kutohudhuria vipindi vya masomo atapewa adhabu ya ndani na asipohudhuria kwa juma zima mfululizo atasimamishwa masomo kwa muda wa siku zisizozidi kumi na nne (14) na atarudi chuoni akiwa*

*ameambatana na mzazi/mlezi wake. Na endapo siku za utoro zitazidi tisini (90) basi mwanachuo huyo atakosa sifa ya kuendelea na masomo na atafutiwa usajiri rasmi.*

3. **Ulevi**

a) Hairuhusiwi kwa Mwanachuo kutumia au kuuza madawa ya kulevya kama vile bangi, milungi na vitu vyote vinavyoendana na hivyo akiwa ndani na nje ya mazingira ya Chuo.

b) Aidha, matumizi ya sigara/pombe hayaruhusiwi katika maeneo ya chuo, madarasani au mabwenini.

c) Pia ni marufuku kwa Mwanachuo kuonekana amelewa. Aidha, ni kosa kwa Mwanachuo kumiliki vileo vya aina yoyote ile bwenini au darasani.

*Mwanachuo atakaye thibitika kutenda kosa la 3 (a) atafukuzwa Chuo mara moja na kupelekwa polisi. Aidha, kwa mwanachuo atakayepatikana na kosa la 3 (b) na (c) atapewa onyo kwa barua, adhabu kali ama kusimamishwa Chuo kwa muda wa siku zisizozidi kumi na nne (14)*

4. **Umiliki wa Silaha**

Ni kosa kwa Mwanachuo yeyote kumiliki au kushikilia silaha zinazoweza kuhatarisha amani ya wanajamuia wa Chuo cha Ualimu Morogoro kama vile kisu, panga, bisibisi n.k.

*Iwapo Mwanachuo atakutwa na kosa hilo ataadhibiwa kwa onyo, kupata adhabu ya ndani itakayopangwa au kupelekwa polisi na kuachishwa masomo/Chuo mara moja.*

5. **Mavazi**

a) Wakati wote ndani na nje ya Chuo, Mwanachuo atatakiwa kuvaa mavazi yenye heshima na safi kulingana na mwongozo wa mavazi.

b) Sare au mavazi rasmi ya Chuo yatavaliwa wakati wote wa vipindi au mwanachuo anapotoka nje ya Chuo. Sketi kwa wanachuo wa kike itapaswa kuwa si pungufu ya **inch 5** kuanzia kwenye magoti kushuka chini na wale wanachuo wa kiume upana wa suruali si chini ya **inch 10**

c) Hairuhusiwi kwa Mwanachuo kuvaa kaptula, malapa, nguo za mipasuo inayovuka magoti, suruali za kubana, sketi fupi na za kubana na kofia katika maeneo ya Chuo. Kwa mwanachuo wa kike ataruhusiwa kuvaa suruali za kitambaa zisizobana na zenye maadili na hasa muda wa kujisomea jioni na siku za mapumziko.

d) Kila mwanachuo atapaswa kuwa na pea moja ya track suit ambayo ataivaa muda wa michezo, muda wa kujisomea usiku na siku moja katika siku za masomo itakayoamuliwa na utawala wa chuo.

*Mwanachuo atakayebainika kukiuka sheria hii atajazishwa fomu ya onyo kali au adhabu za ndani au kusimamishwa masomo kwa muda usiopungua siku 21.*

6. **Unyanyasaji wa kijinsia**

Unyanyasaji wa kijinsia au wa kimaumbile katika Chuo cha Ualimu Morogoro wa aina yoyote haukubaliki. Hii ni pamoja na;

a) Kumlazimisha mtu kwa kumtaka kimapenzi kwa kutumia maneno, ishara, picha au vitisho vyenye maudhui ya kimapenzi au kumsababishia mwanachuo kukosa amani ama kushindwa kuendelea na masomo yake.

b) Kutumia ishara za kufanya mapenzi katika mazingira ya Chuo au kumshikashika mtu bila ridhaa yake

c) Kumkashifu au kumnyanyapaa mtu yeyote kutokana na maumbile aliyonayo au ugonjwa alionao.

*Kwa Mwanachuo atakayebainika kuwa na kosa hilo la unyanyasaji wa kijinsia atasimamishwa kuendelea na masomo au kusimamishwa kwa muda usiozidi siku ishirini na moja (21)*

7. **Wizi na ugomvi**

a) Ni kosa kwa mwanachuo yeyote yule kujihusisha na vitendo vya wizi na ugomvi

b) Ni kosa kwa mwanachuo kushirikiana na mwanachuo mwingine kujihusisha na wizi au kununua vitu vilivyoibwa kwa mtu mwingine.

c) Ni kosa kwa mwanachuo yeyote yule kujihusisha katika kushawishi ugomvi ndani au nje ya mazingira ya Chuo.

d) Na Mwanachuo atakaefanya vitendo vyovyote vitakavyopelekea kumdhuru mtu na mali yake katika mazingira ya Chuo, hii ni kama Mwanachuo dhidi ya Mwanachuo mwenzake, mfanyakazi na mwanajumuiya ya Chuo cha Ualimu Morogoro au nje atakuwa amevunja sheria hii.

*Kwa Mwanachuo atakayebainika kuwa ameshiriki kuvunja sheria hii atasimamishwa masomo kwa muda usiozidi siku ishirini na moja (21), kulipa vitu alivyoiba au kufukuzwa chuo.*

8. **Ubakaji, ulawiti na usagaji/ushoga**

a. Ubakaji, ulawiti na usagaji/ushoga haviruhusiwi mahali popote pale.

b. Hairuhusiwi wanachuo wawili kulala kitanda kimoja

*Mwanachuo atakeyebainika kujihusisha na vitendo hivyo atasimamishwa masomo au kupelekwa polisi au kutumikia adhabu zote mbili kwa pamoja*

9. **Kukataa wito/kugoma/mgomo**

   a. Mwanachuo kukataa kuhudhuria vikao au mikutano halali iliyoitishwa na uongozi wa Chuo, kukataa kuitika wito wa mfanyakazi halali wa Chuo cha Ualimu Morogoro au kutoshiriki katika kazi zilizopangwa na uongozi wa Chuo, serikali ya Wanachuo au wakufunzi wa Chuo cha Ualimu Morogoro ni kosa

   b. Ni kosa kushawishi au kujenga mazingira mbalimbali ya ushawishi kwa wanachuo wengine kushiriki kukataa wito/kugoma.

      *Mwanachuo atakaekutwa na kosa hili atapewa barua ya onyo, atapata adhabu ya ndani ikiwemo kusimamishwa masomo kwa kipindi kisichozidi siku 21*

10. **Vifaa na matumizi ya mali ya umma**

    a. Hairuhuisiwi kuhamisha samani za Chuo cha Ualimu Morogoro (viti, godoro, meza n.k) kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine bila ya kibali kutoka uongozi wa Chuo cha Ualimu Morogoro.

    b. Hairuhusiwi kwa mwanachuo kupoteza au kuharibu kifaa/mali ya chuo kwa uzembe au kwa kukusudia ikiwa ni pamoja na kuandika au kuchora kuta bila ya kibali kutoka katika uongozi wa chuo.

    c. Ni marufuku kwa mwanachuo kupeleka chakula bwenini. Chakula chote kitaliwa bwaloni au canteen, isipokuwa kwa idhini maalum kutoka ofisi ya uadili.

       *Kwa Mwanachuo atakayetenda kosa hili atajazishwa fomu ya onyo au karipio kwa mara ya kwanza na kupewa adhabu ya ndani, kulipa fidia na akirudia kosa hilo atasimamishwa masomo kwa siku zisizozidi ishirini na moja (21) na kulipa mali iliyopotea au kuharibika.*

11. **Matumizi mabaya na hatarishi ya mali na miundombinu**

    Ni kosa kufanya matumizi mabaya na hatarishi ya mifumo ya umeme na maji katika Chuo cha Ualimu Morogoro. Matumizi hayo ni kama vile; kuunganisha nyaya za umeme kinyume na mfumo uliowekwa katika jengo husika, matumizi ya mishumaa, chemli, jiko au birika za umeme, vifaa vya kukaushia nywele (drier) na uchafuzi wa vyanzo vya maji, kuchafua kuta za bweni/darasa.

    Ni marufuku kwa Mwanachuo kupeleka chakula bwenini. Chakula chote kitaliwa bwaloni au canteen, isipokuwa kwa idhini maalum kutoka ofisi ya uadili.

    *Kwa kosa hili mhusika atatakiwa kulipa au kugharamia matengenezo ya hasara/uharibifu/madhara aliyoyasababisha au kujazishwa fomu ya onyo au kusimamishwa masomo kwa kipindi kisichozidi siku ishirini na moja (21) au adhabu zote kwa pamoja.*

12. **Matumizi mabaya ya lugha**

Matumizi ya lugha ya matusi, kejeli au kutishia zinazofanywa na Mwanachuo dhidi ya mfanyakazi yeyote wa Chuo, viongozi wa serikali ya wanachuo kwa lengo la kukwamisha asikamilishe wajibu wake hazitakubalika. Aidha, lugha za namna hiyo hazitakiwi pia kutumiwa na Mwanachuo dhidi ya mgeni au mwanajumuiya wa Chuo cha Ualimu Morogoro.

Hairuhusiwi kwa Mwanachuo kuandika au kuchora picha zinazoashiria matusi, kejeli, kashfa au udhalilishaji juu ya viongozi wa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, viongozi wa dini, mfanyakazi au wafanyakazi wa Chuo cha Ualimu Morogoro au mtu mwingine yeyote ndani na nje ya Chuo cha Ualimu Morogoro kwa njia yoyote ile. Aidha, ni kosa kuonesha dharau kwa alama za Taifa.

*Mwanachuo yeyoye atakayefanya kosa hili chini ya sheria hii atasimamishwa masomo kwa kipindi kisichozidi siku ishirini na moja (21).*

13. **Ushawishi**

a. Hairuhusiwi Mwanachuo kuchochea, kushawishi au kushiriki migomo.
b. Ni kosa kushawishi au kujenga mazingira mbalimbali ya ushawishi kwa wanachuo wengine kutenda kosa.

*Mwanachuo atakaye shiriki kosa hilo atasimamishwa masomo kwa muda wa siku 21 au kufukuzwa Chuo.*

14. **Sheria ya Mawasiliano**

a. Ni kosa kwa mwanachuo yeyote yule kutumia mitandao ya kijamii kwa kuandika pamoja na kurusha machapisho mbalimbali kinyume cha sheria, kanuni na taratibu za chuo na nchi kwa ujumla.
b. Hairuhusiwi kwa mwanachuo kutoa taarifa zozote za chuo kwa mtu yeyote bila kuruhusiwa na uongozi wa chuo.
c. Ni kosa kutoa habari au taarifa za mwanachuo mwingine kwa mtu mwingine kuhusiana na afya yake, maisha yake au mambo mengine binafsi bila idhini yake mwenyewe.
d. Ni kosa kuweka picha za utupu zako au za mwenzako kwenye mitandao

*Mwanachuo atakayebainika kushiriki kosa hili kwa mujibu wa sheria hii atasimamishwa masomo kwa muda wa siku zisizozidi ishirini na moja (21), kupelekwa polisi au kufukuzwa Chuo.*

15. **Mahusiano**

a. Ni kosa kwa mwanachuo yeyote yule kuonyesha dalili kwa namna yoyote ile ya kuwa na mahusiano ya kimapenzi/kuishi kama mke na mume na mwanachuo mwenzake au mfanyakazi wa Chuo Cha Ualimu Morogoro au mtu mwingine yeyote.

i. *Mwanachuo atakayebainika* kuwa na mahusiano ya kimapenzi/kuishi kama mke na mume *atasimamishwa masomo kwa muda wa siku zisizozidi ishirini na moja (21).*

ii. *Na endapo mwanachuo atabainika kuwa na ujauzito na aliesababisha ni mwanachuo mwenzake, basi wanachuo wote watalazimika kuahirisha mwaka wa masomo ili kupata muda wa kwenda kuhudumia ujauzito huo na hatmae kulea mtoto.*

16. **Uingiaji katika mabweni**

a. Hairuhusiwi kwa mwanachuo yeyote yule kuingia bweni lisilo lake bila kibali toka kwa mlezi wa bweni husika

b. Mwanachuo wa kike/kiume haruhusiwi kuingia kwenye bweni la wanachuo wa jinsia nyingine bila kibali kutoka ofisi ya Uadili.

c. Hairuhusiwi kwa mwanachuo yeyote yule kumpeleka/kumkaribisha mgeni asiyekuwa mwanachuo bwenini.

*Mwanachuo atakayethibitika kutenda kosa hili anaweza kupewa adhabu za ndani au kusimamishwa masomo kwa kipindi kisichozidi siku saba (7) au adhabu zote kwa pamoja.*

Mimi:______________________________ Mchepuo__________Darasa__________ nimezisoma sheria za Chuo cha Ualimu Morogoro na kuzielewa. Naahidi kuishi kwa kuzifuata kwa muda wote nitakao kaa hapa Chuoni.

Saini: ______________________________ Tarehe: _________________________